Wassira aishika pabaya Chadema

Kisima Cha Maarifa

# FIKRA PEVU

fikrapevu | @fikrapevu | @fikrapevu

Tovuti: www.fikrapevu.co.tz | ISSN 3456-17 Toleo Na.16 Fikra Pevu Jumatatu Februari 10, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100





# Dk.Biteko awalingania Waislamu kuhifadhi Qur'aan Tukufu

UK 2

>> Awaasa Waislamu kuyaenzi mashindano ya Qur'aan

>> Ampongeza Sheikh Kishk,Mashindano kufanyika Machi 16



UK 3

## Buriani Sam Nujoma 1929-2025

## Shida ya maji Tabata, Segerea, sasa basi

UK 2



## Bodi wakala wa vipimo wampongeza Dk.Samia

UK 3

# Dk.Biteko awalingania Waislamu

Na Mwandishi Wetu

**NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati,Dkt. Doto Biteko amewaasa waislamu nchini kuendelea kumcha Mungu na kutenga muda wa kujifunza na kuisoma Qur'aan Tukufu ambayo itawafunza mambo mema yaliyoelekezwa na Mwenyezi Mungu.**

Dkt. Biteko amesema hayo jana jijini Dar es salaam wakati akizindua Mashindano Makubwa zaidi ya Qur'aan Tukufu Ulimwenguni 2025.

" Nawaomba msivunjike moyo akitokea mwenye tafsiri tofauti nyie msivunjike moyo wala kukatishwa tamaa bali mfanye mashindano haya yawe kinara na kuutangaza uislamu katika ulimwengu," amesema Dkt. Biteko.

Pia amewahimiza kumuomba Mungu ili Qur'aan iwanyanyue na isiwabwage katika shughuli mbalimbali wanazofanya kama kaulimbiu ya mwaka huu inavyosema " Qur'aan Ikunyanyue, Isikubwage".

Alisema,Qur'aan inatoa funzo kwa watu na kuwa waasisi wake waliyaanzisha kwa ngazi ya madrasa lakini baadaye kutokana na umuhimu wake yakavutia wengi zaidi na kuwa mashindano ngazi ya mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi kuwa ya Afrika Mashariki, Bara la Afrika na kisha kufikia ngazi ya kuwa mashindano ya Ulimwengu.

" Mashindano haya mbali na kuwa yanachochea usomaji wa Qur'aan Tukufu na hivyo kujenga uelewa wa hofu ya Mwenyezi Mungu lakini pia yanaitangaza Tanzania katika taswira chanya," amebainisha Dkt. Biteko.

Alisema,kuwa Nabii Musa aliwalingania watu wake kwa kutumia muongozo kutoka katika Taurati, Nabii Daudi yeye akatumia Zaburi, Nabii Issa (Yesu) akatumia Injili na Mtume Muhamad swalla Ilahu alayhi wasallam akatumia Qur'aan tukufu kuwalingania watu wa umma wake.

"Kimsingi vitabu hivi vya muongozo vinamfundisha binadamu tabia njema na kumsihi kuzishikilia na kumuonesha tabia zisizofaa na kumuasa kukaa mbali nazo."

Dkt. Biteko amerejea aya katika Qur'aan tukufu sura ya 35, Surat Faatir, aya ya 28 "... kwa hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni".

Amefafanua " Aya hii ina maanisha kuwa wale waliopata ujuzi na mafundisho ya Mwenyezi Mungu ambayo yanapatikana katika Qur'aan tukufu na kuyazingatia yale waliyojifunza ndio wanaofika daraja la uchamungu."

Vilevile, Dkt. Biteko ameipongeza Taasisi ya Al- Hikma kwa jitihada zake za kukuza Mashindano ya kuhifadhi Qur'aan Tukufu ulimwenguni.

Mkurugenzi Mkuu wa Al- Hikma na Mwenyekiti wa Mashindano ya Qur'aan Tukufu Ulimwenguni, Sheikh Nurdin Kishk amesema kuwa mashindano hayo yameendelea kukua kila mwaka kutokana na mapenzi ya kuhifadhi Qur'aan.

Aidha, ameishukuru Serikali kwa ushirikiano wake na kwa kuridhia mashindano hayo kufanyika katika Uwanja wa Taifa Machi 16, 2025 ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

" Mashindano haya yanayofanywa na Al- Hikma Foundation yameweka alama ambayo haitafutika na mataifa mbalimbali yameanza kuyaiga. Pia, Mashindano Makubwa Zaidi ya Qur'aan Tukufu Afrika sasa yatajulikana kama Mashindano Makubwa Zaidi ya Qur'aan Tukufu kwa Mabara yote ya Ulimwengu ," amesema Sheikh Kishk

Akizungumza kwa niaba ya Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ali Ngerukwa alisema kuwa Mufti Mkuu yupo tayari kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo ya Ali- Hikma katika kutekeleza shughuli zao.

# Shida ya maji Tabata,Segerea, Kinyerezi sasa basi

Na Juma Kasesa

ZIMESALIA siku 10 tu kabla ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam(DAWASA) kumaliza tatizo la maji kwa wakazi wa Tabata,Segerea na Kinyerezi.

Wakazi wa maeneo wamekuwa kwenye kadhia ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu lakini sasa ni rasmi tatizo linakwenda kumalizika baada ya DAWASA kukamilisha mradi wa upelekaji maji kwa maeneo hayo kwa asilimia 99.

Kaimu Mkurugenzi wa DAWASA,Mkama Bwire amewaeleza wananchi wa maeneo hayo kwamba kuanzia Februari 20 mwaka huu watafungulia rasmi maji ili kuwaondolea kero hiyo ya muda mrefu.

Bwire alisema,serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuwaondolea kero ya maji Wananchi wake kwa kutoa fedha za ukamilishaji miradi mbalimbali ikiwemo huo wa ambao unakwenda kuwa mwarobaini wa tatizo la maji kwa wakazi wa maeneo hayo.



# Wassira aishika pabaya Chadema

Na Mwandishi Wetu

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Stephen Wasira amevionya vyama upinzani kuacha kuwatumia vijana kutoka mkoani Mara kama nguvu kazi ya kufanya vurugu katika maeneo mbalimbali.

Wasira ametoa onyo hilo jana alipokuwa akizindua ofisi ya CCM Kata ya Nyakonga wilayani Tarime, Mkoa wa Mara.Alisema CCM ina mipango mizuri kuhakikisha vijana hao wanatumia nguvu zao kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kujikwamua dhidi ya umasikini.

'Nataka niwaambie wananchi wa Tarime CHADEMA wakitaka kufanya fujo mahali popote wanakuja kuchukua vijana Tarime...wanapelekwa kufanya fujo kama majeshi ya kukodi, wakitaka kufanya fujo Mbeya wanakuja, Tarima, wakitaka kufanya fujo sehemu Tarime.

"Tunawaambia vijana wa Tarime wana mvua wana jua na Tarime panalimika, kila kitu kinaota tuwasaidie vijana wa Tarime watumie fursa zilizopo...tunawaambia CHADEMA muache kuja kuchukua vijana Tarime, sisi sio eneo la mapambano, vijana wetu sio wa kukodisha kwenda katika mapambano, nasema kama mzee wa Tarime waache kuja kuchukua vijana wa Tarime.

Wasira aliwataka vijana wasikubali kuchukuliwa na kutumika katika vurugu kwa kuwa wakienda huko hupigwa, kuumizwa na hata kupata ulemavu kisha kurudishwa Tarime wakiwa na hali mbaya.

"Nasema kama mzee wa Tarime, Mzee wa kimila, muache mambo haya mimi najua yanafanyika siku nyingi," alisema.



# Buriani Sam Nujoma 1929-2025

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa kwanza wa Namibia huru, Sam Nujoma, amefariki dunia akiwa na miaka 95 katika mji mkuu wa Windhoek, kiongozi wa sasa wa nchi hiyo ametangaza.

Nujoma aliongoza vita vya muda mrefu vya kudai uhuru kutoka kwa Afrika Kusini mwaka 1990 baada ya kusaidia kupatikana kwa vuguvugu la ukombozi la Namibia lililojulikana kama South West Peoples' Organization (Swapo) miaka ya 1960.

Baada ya uhuru, Nujoma alikua rais mwaka 1990 na aliongoza nchi hadi 2005.

Nujoma alikuwa amelazwa hospitalini kwa muda wa wiki tatu zilizopita kutokana na ugonjwa ambao "hakuweza kupona", Rais wa Namibia Nangolo Mbumba alisema katika taarifa yake akitangaza kifo hicho kwa "huzuni na masikitiko makubwa".

Aliongeza: "Baba yetu mwanzilishi aliishi maisha marefu na yenye matokeo ambayo alitumikia kipekee watu wa nchi yake anayoipenda."

Nujoma alistaafu kama mkuu wa nchi mwaka 2005, lakini aliendelea kukiongoza chama hicho kabla ya kung'atuka mwaka 2007 kama rais wa chama tawala cha Swapo baada ya kukiongoza kwa miaka 47.

# Bodi wakala wa vipimo wampongeza Dk.Samia

Na Veronica Simba

MKANDARASI wa Jengo la Wakala wa Vipimo(WMA)leo anarajiwa kukabidhi jengo la Ofisi Kuu ya Wakala huyo lililo jijini Dodoma.

Februari 7 mwaka huu ya Bodi ya Wakala wa vipimo ilifanya ziara ya kukagua ujenzi wa jengo hilo na kuridhishwa na kazi iliyofanywa na mkandarasi ambaye aliahidi Februari 10 kukabidhi wahusika.

Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Eliza Mwakasangula alisema hatua iliyofikiwa katika ujenzi husika, imewadhihirisha pasipo shaka kuwa litakabidhiwa katika hali ya ukamilifu kama walivyoliona.

"Tumeridhishwa sana na kazi iliyofanywa na Mkandarasi kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi. Kinachofanyika sasa ni kukamilisha kazi ndogo ndogo zilizosalia. Kwa hatua iliyofikiwa, hatuna shaka kufikia Febaruari 10 mwaka huu ambayo ndiyo siku ya kukabidhiwa rasmi, Jengo litakuwa limekamilika kwa viwango stahiki," amesema.

Aidha, Prof. Mwakasangula amemshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga bajeti ya ujenzi wa Jengo hilo ambalo limegharimu takribani shilingi bilioni 6.2 ambazo ni fedha za ndani.

Pia, amemshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Selemani Jafo na Menejimenti yake pamoja na kumpongeza Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla na Menejimenti yake yote kwa usimamizi mzuri wa jengo hilo.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu Kihulla amewaeleza waandishi wa habari kuwa kukamilika kwa jengo hilo kutatatua changamoto mbalimbali za kiofisi.

"Tumeanza na jengo hili lakini matarajio ni kujenga katika maeneo mengine ili mazingira ya kiofisi kwa wateja wanaokuja kupata huduma yawe mazuri lakini na kwa watumishi pia."

Ametaja faida nyingine ya kukamilika kwa jengo hilo kuwa ni kuwezesha vifaa vya kitaalamu kukaa katika mazingira ambayo ni mazuri ili kuendana na usahihi wa kimataifa.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Ukandarasi ya Mohamed Builders inayojenga jengo hilo, Jaffar Mohamed amemhakikishia Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi hiyo kuwa watakabidhi jengo hilo likiwa limekamilika kama ilivyopangwa. Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo Makao Makuu, ambao kwa sasa wako Dar es Salaam, wanatarajiwa kuhamia Dodoma hivi karibuni baada ya kukamilika kwa Jengo hilo ikiwa ni kutimiza maelekezo ya Serikali yanayozitaka Taasisi na Mashirika yote ya Umma kuhamia Makao Makuu ya nchi, Dodoma.

# Waziri Kikwete akabidhi vijana Hundi ya Tsh.Milioni 700

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete amekabidhi hundi ya shilingi Milioni 730 kwa Vikundi 74 vya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu kutoka Halmashauri ya Muheza, jijini Tanga ambayo inatokana na mikopo ya asilimia 10 kupitia mapato ya ndani.

Akizungumza wakati wa kukabidhi hundi hiyo jana,Kikwete,alisema,utaratibu wa kutoa Mkopo kwa makundi hayo umekamilika hivyo kwa sasa kikundi au mtu mmoja anayekidhi vigezo ataweza kunufaika na Mkopo huo.

Ridhiwani amebainisha kuwa, vikundi vilivyonufaika na mkopo huo vimepatiwa elimu ya ujasiriamali na matumizi mazuri ya pesa ili kukua zaidi na kuepuka changamoto zilizokuwepo awali ikiwemo kubadilisha matumizi ya Mkopo huo na kufanyia mambo mengine hivyo kupelekea wakopaji kutorejesha pesa hizo kwa wakati au kushindwa kulipa kabisa.

Alisema Serikali ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuwezesha makundi mbalimbali mikopo yenye riba nafuu ikiwemo mikopo ya asilimia 10.Katika hatua nyingine,Ridhiwani aliwataka wanufaika wa mkopo huo kurejesha pesa hizo kwa wakati ili wengine waweze kukopeshwa.



# Mitano tena inamuhusu Dk.Samia

Na Lucas Hebel Mwashambwa

HUO ndio uamuzi kutoka katika mioyo ya mamilioni ya wafuasi, wakereketwa,mashabiki na wanachama wa CCM Nchini kwote.Ni lazima tumpe Miaka mitano Mama yetu Mpendwa na Jemedari wetu kipenzi Daktari Mama Samia Suluhu Hasssan shujaa wa Afrika, jasiri muongoza njia, simba wa nyika, komandoo wa vita, nyota ya matumaini na nuru ya wanyonge kuliongoza Taifa letu.

Ni mitano mingine kwa sababu sote tumeona na kushuhudia juhudi zake katika kuleta maendeleo kwa Taifa letu,tumeona uchapakazi wake,tumeona umadhubuti wake katika kushughulikia kero na changamoto mbalimbali,tumeona ushupavu wake,uimara wake na uhodari wake katika kuwainua watanzania.


Tumeona namna alivyoleta Matumaini palipo kuwa na kukata tamaa,tumeona akileta nuru na mwanga palipokuwa na giza,akionyesha njia na muelekeo mahali palipokuwa na njia panda katika mioyo na akili za watu.tumeona akifungua fursa kwa watu.tumeona na ndani ya muda mfupi kabisa akijenga uchumi imara , shirikishi na wenye kugusa maisha ya watu.

Tumeona Taifa likiendelea kuwa lenye amani na utulivu.Tumeona namna alivyotuunganisha watanzania,tumeona namna alivyojenga kuaminiana na umoja wa kitaifa ,tumeona akileta heshima mahali palipokuwa na kudharaulika,tumeona namna mama huyu Mwenye moyo wa upendo ,huruma, ukarimu na utu namna alivyo msikivu, Mnyenyekevu na mzalendo wa kweli kwa Taifa letu.

Tumeona namna alivyomfikia kila mtanzania kwa huduma bora za kijamii na fursa za kiuchumi na sote tumeona namna anavyopambana kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma wala kusahaulika wala kudidimizwa wala kukatishwa tamaa .tumeona ambavyo amekua muwezeshaji wa watanzania wote.

Ndio Maana tunasema liwe jua iwe Mvua ni lazima tumpatie miaka mitano ya kuliongoza Taifa letu kwa muhula wa pili. sisi ndio wenye Nchi na tunajuwa ni nani anatufaa kutuongoza na kwa pamoja tunasema ni Daktari Mama Samia Suluhu Hasssan aliye chaguo la Mioyo yetu na mwenye uwezo wa kutuongoza watanzania.

Kazi iendelee, Mama Ametufikia na kuwafikia watanzania kwa utumishi wake uliotukuka wa kugusa maisha ya watanzania wanyonge wasio na Sauti.







# Upinzani uko usingizi, CCM wanachanja mbuga

**WAKATI vyama vingine vya kisiasa viko usingizini na vingine vikibabaika na mjadala wa kuunganisha nguvu ama laa, Chama Cha Mapinduzi(CCM) tayari kimeshakamilisha maandalizi muhimu ya ndani kuhusu uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu.**

Watanzania wanatarajia kupiga kura kuchagua Rais, Wabunge na Madiwani Oktoba mwaka huu ambapo ni CCM pekee iliyoonesha kuwasha taa ya kijani kuashiria kuchapa mwendo kukimbizana na mchakato wa uchaguzi.

Rafiki zangu Chadema wanaotajwa kama chama Kikuu cha upinzani ni kama bado wako kwenye usingizi mzito.Baada ya zoezi la uchaguzi la kupata viongozi wao wapya wa kitaifa wamevuta shuka na kuchapa usingizi.Hawasikiki chochote kuhusu mikakati yao nani atakuwa mgombea urais wao.

Ni kama vile wamepigwa na kitu kizito kichwani baada ya CCM kumuanika Dk.Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dk.Emmanuel Nchimbi akiwa ndiye mgombea mwenza wake.

Nini kimeifanya Chadema na vyama vingine kumezwa na upepo wa CCM kupata mgombea Urais wake mapema. Walikua wanasubiria nini?Iwe nini?Walau rafiki zangu ACT wazalendo wao nimesikia wamefungua pazia la wanachama kuchukua fomu ya kugombea urais.

Nani anaweza kuwa mgombea wa ACT na kumtikisa Dk.Samia?Jibu ni rahisi tu hakuna. Twende kwa Chadema ni kama na wao hawana mgombea mwenye mvuto licha ya kwamba mtu pekee ambaye amekuwa akitajwa kusimama kwa tiketi ya chama hicho ni Tundu Lissu.

Swali hapa ni je akiteuliwa kugombea ana hoja gani zenye mashiko kumkabili Dk.Samia?

Ni suala la muda tu wa kisheria na kikatiba ndio unasubiriwa.Na hii ni ishara ya wazi na maandalizi kabambe ya ushindi wa kishindo mathalani kwenye nafasi ya urais, ambayo tayari mgombea urais Dk.Samia Suluhu Hassan na mgombea mwenza wake Dk.Emmanuel Nchimbi, wanafahamika kwa waTanzania wote, wanakubalika na kuaminika kwa wananchi kuliko mwanasiasa yeyote nchini Tanzania.

Kwa uzoefu wako katika siasa za Tanzania, na kwa kuzingatia hali ya siasa na kukubalika kwa wagombea hao makini wa chama tawala, unadhani CCM inaweza kupata ushindi wa chini ya 90% kweli kwenye uchaguzi Oktoba mwaka huu??

**Mungu Ibariki Tanzania**



# Naitabiria Tanzania itakuwa ghala la chakula Afrika

**Na Emmanuel Mhando**

SIDHANI kama kuna mtu atabisha kwamba, kwenye nchi hii hakuna wakati sekta ya kilimo imepata mazingatio makubwa sana kuliko wakati wowote ule kwenye historia ya nchi yetu.

Ushahidi wa kwanza wa hoja yangu ni Rais Samia Suluhu kuongeza bajeti ya kilimo kwa zaidi ya asilimia 200, kutoka TZS Bilioni 294 2021/22 hadi TZS Trilioni 1.3 2024/25. Kiwango cha ongezeko hili, hakijapata kutokea kwenye ardhi ya Taifa lote chini ya kiongozi yeyote.

Lengo na mapinduzi haya ni nini? Kwanza, ni kufanya sekta hii ichangia 10% kwenye Pato la Taifa ifikapo 2030, kuongeza ajira kwa kuzalisha ajira mpya zaidi ya milioni 3 kwa vijana ifikapo 2025 (BBT), kuifanya Tanzania kama muuzaji mkubwa wa chakula barani Afrika na duniani na pia, kutengeneza mazingira ya kuwa na chakula cha kutosha nchini.

Kutoka na uwekezaji huu, muda huu Tanzania ina utoshelevu wa chakula wa zaidi ya asilimia 124, kiwango kikuwa zaidi kuwahi kutokea nchini. Hii imetokana na Rais Samia Suluhu kusimamia ujenzi wa vihenge na maghala mapya ya kuhifadhia chakula katika Kanda nane nchini zenye hifadhi ya chakula ambazo ziko chini ya NFRA.

**TZS Bilioni 294 2021/22 hadi TZS Trilioni 1.3 2024/25. Kiwango cha ongezeko hili, hakijapata kutokea kwenye ardhi ya Taifa lote chini ya kiongozi yeyote.**

Ili ujue kwamba Rais Samia yuko serious kwenye kilimo, bajeti ya utafiti na uzalishaji wa mbegu imeongezwa kwa asilimia 250, huku bajeti ya kuhudumia ma afisa ugani vijijini ikipata kutoka TZS 600 milioni hadi TZS Bilioni 17.7, hakika haya ni mapinduzi makubwa sana na hayapaswi kupuuzwa hata kidogo.

Baada ya miaka kadhaa mbele, naona kabisa ndogo ya kuifanya Tanzania kuwa the 'Africa Food Basket' inakwenda kutimia, tumeongeza eneo la umwagiliaji na hadi kufikia 2025 eneo litakuwa limefikia hekta zaidi ya 1,000,000.

Kuna skimu mpya za umwagiliaji zaidi ya 20 zinajengwa muda huu na serikali inazidi kuimarisha vyama vya ushirika nchini na hivi majuzi kwenye maandimisho ya siku ya Nane Nane, Mama amekabidhi matrekta mapya 500 na Powertillers 800 kwa wakulima, lengo ikiwa ni matrekta 10000 na powertiller idadi hiyohiyo, zisambazwe kwa wakulima nchi nzima kabla ya kufika 2030.



# Rais Samia atashinda uchaguzi kwa makubwa aliyoyafanya

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan ni kiongozi wa kipekee ambaye amebeba matumaini makubwa ya Watanzania.Utendaji kazi wake umejikita katika kuimarisha uchumi, kuleta maendeleo, na kuhakikisha mshikamano wa kitaifa.

Kama mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameonesha kuwa uongozi bora haupimwi kwa jinsia, bali kwa maono, uchapa kazi wake na utekelezaji wa ahadi kwa vitendo.

Katika kipindi chake cha miaka 4, Rais Samia amesimamia kukamilika na uendelezaji wa miradi mikubwa kama Reli ya Kisasa (SGR), Bwawa la Umeme la Julius Nyerere ,Uwekezaji mkubwa Bandari ya Dar es salaam, Uwanja wa Ndege wa Msalato, Daraja la Kigongo Busisi, na Upanuzi wa Huduma za Maji Safi na Umeme Mijini na Vijijini.

Ameboresha sekta za afya na elimu kwa kujenga Shule na Hospitali, kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba, na kuboresha maisha ya Wafanyakazi. Jitihada zake za kuvutia wawekezaji zimeimarisha Uchumi wa Taifa na kupanua fursa za ajira kwa Watanzania walio wengi.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema Mwalimu Nyerere alitambua uwezo wa wanawake katika kuleta mabadiliko. Kauli yake imejidhihirisha kupitia uongozi wa Rais Samia, ambaye amekuwa mfano bora wa utekelezaji wa maono hayo kwa vitendo.

Rais Samia mara kwa mara amesisitiza kuwa wanawake si wanyonge. aliwahi kusema; Kupitia hotuba zake na vitendo vyake, amewahamasisha wanawake kote nchini kushiriki kikamilifu katika maendeleo. Pia ameongeza uwakilishi wa wanawake kwenye nafasi za uongozi serikalini na taasisi mbalimbali.

Uongozi wake umethibitisha kuwa CCM ni Chama kinachojali maslahi ya wananchi. Miradi inayotekelezwa ambayo imegusa maisha ya watu wa kawaida ni udhihirisho wa dhamira ya Chama ya kuleta maendeleo jumuishi. Rais Samia ameimarisha imani ya Watanzania kwa CCM kupitia uwajibikaji na utekelezaji wa ahadi za Chama.

Rais Samia ni mfano bora wa uongozi thabiti unaothamini mshikamano, maendeleo, na uwajibikaji. Ameonyesha kuwa wanawake ni nguzo muhimu ya maendeleo ya Taifa. Kwa utendaji wake wa bidii na maono amekuwa turufu ya CCM kwa Watanzania na kielelezo cha matumaini kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2025.

CCM kwa aina ya Mgombea waliomteua haina shaka kuwa itashinda kwa kishindo na kuweka historia nyingine kwa kuwa na Mgombea Mwanamama wa Kwanza aliyeshinda Urais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliko vipindi vingine vyote vya uongozi katika historia ya Tanzania.





# Jumuiya ya EAC,SADC katika mtihani wa kutatua mgogoro wa DRC

KUFUATIA gharama kubwa wanayoilipa wakazi wa maeneo ya Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, bila shaka macho, masikio na matumaini yao yote yamekuwa jijini Dar es Salaam kwa siku ya Ijumaa na Jumamosi.

Viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na ile ya Kusini mwa Afrika (SADC) watakuwepo nchini Tanzania katika mazungumzo ya kujaribu kuutatua mgogoro huo. Mawaziri wametangulia kukutana siku ya Ijumaa halafu Marais wanakutana Jumamosi.

Lakini swali kubwa ni; jumuiya hizi, zina meno ya kuutatua mgogoro huo?

Mtaalamu wa migogoro na usuluhisi na Balozi Dk.Mohamed Omar Maundi anasema moja ya changamoto kubwa ya kuumaliza mgogoro wa Congo ni idadi ya wahusika wa mgogoro wenyewe

"Sasa hivi tunapozungumzia mgogoro wa Congo, hatuwazungumzii Wacongo wenyewe, tunawazungumzia na wadau wengine ambao mgogoro wa Congo umewahusisha. Nchi Jirani, maslahi ya watu wengine nje ya Afrika, kuna wadau wengi katika mazingira ya wadau wa Congo," anasema Dk. Maundi

Mkutano uliofanyika uliopita ni kwasababu unajumuisha jumuiya za kanda mbili tofauti kujaribu kutafuta suluhisho la mgogoro wa nchi moja.Imebidi mkutano huu ufanyike si tu kwasababu DRC ni mwanachama wa jumuiya zote hizi mbili, lakini pia inazungukwa na nchi nyingi za upande wa Mashariki na mbili za Kusini, hivyo mambo yakiharibika DRC, basi madhara yatasambaa kirahisi kwa nchi zote hizi za jirani

Kihistoria, Umoja wa Mataifa ndio umekuwa ukibeba jukumu la kutatua migogoro duniani kote.Lakini tangu miaka ya 90', Umoja wa Mataifa ulilemewa na jukumu hili, ukaanza kulipeleka zaidi kwa jumuiya za kikanda, hasa kwa nchi za Ulaya Asia na Afrika

Hata hivyo, jumuiya za barani Afrika zimekuwa na mafanikio kidogo kuliko zilivyotarajiwa.Jumuiya ya Afrika Magharibi, ECOWAS, ilisifiwa baada ya kuzisimamishia uanachama nchi tatu – Mali, Niger na Burkina Faso – kufuatia mapinduzi ya kijeshi dhidi ya serikali zilizokuwepo madarakani

Lakini jumuiya za SADC na EAC, hazina rekodi ya kusisimua sana juu ya uwezo wao kutatua changamoto za kiusalama na kisiasa zinazotokea katika nchi wanachama wao

Msumbiji ilipoanza kukabiliwa na wanamgambo wa Al Shabaab, kwa mfano, SADC ilitarajiwa ingeisaidia Msumbiji, lakini ni Wanajeshi wa Rwanda ndio wameonekana kufanikiwa zaidi kuwakabili wapiganaji wa Al Shabaab

Hata huu mgogoro unaoendelea hivi hasa huko DRC, wengi wanaamini, kama Jumuiya EAC ingekuwa na uwezo na nyenzo za kutosha, ingeweza kusaidia kuutatua kabla ya kufikia katika hatua iliyofikiwa hivi sasa.

Kwa ujumla, madhumuni ya uanzishwaji na muundo wa jumuiya hizi ni sababu kubwa ya kwanini jumuiya zingine zinafanikiwa zaidi kuliko zingine katika kudhibiti migogoro

Wasomi mbalimbali wanaona mantiki ya jumuiya hizi mbili kushughulikia mgogoro huu, lakini wanatahadharisha juu ya vigingi vingi vya kuvuka kabla mafanikio ya suluhisho hayajafikiwa

"Ingawa kuna uungwaji mkono mkubwa kwa juhudi za jumuiya za kikanda, tofauti kubwa za mbinu haziwezi kupuuzwa.Nchi kadhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zinachukulia mazungumzo kati ya Kinshasa na M23 kuwa njia pekee ya kupiga hatua katika kutatua tofauti zao, na zinajiepusha kusema hadharani kuhusu ushiriki wa Rwanda (katika mgogoro huo).

Kwa upande mwingine, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ilishutumu mashambulizi ya hivi karibuni ya M23 dhidi ya SAMIDRC, ilitaka Rwanda ijiondoe, na ilisisitiza tena uungwaji mkono kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)," wanaandika wanazuoni Bram Verelst na Nicodemus Minde wa Institute for Security Studies

Kwa maneno mengine, wakati baadhi ya nchi wanachama wanasisitiza M23 ni Wakongo, na kwamba madai yao yashughulikiwe kisiasa, DRC na Burundi inakiangalia kikundi hiki kama waasi wanaotumika na Rwanda kuhatarisha amani ya Congo na hivyo namna pekee ya kushughulika nao ni kupitia nguvu ya kijeshi.

Utofauti wa itikadi miongoni mwa wanachama wa jumuiya hizi juu ya mzizi wa tatizo ambao ni utaifa wa waasi wa M23 ni kikwazo kikubwa na cha msingi katika kutatua mgogoro huu.Lakini kuna hali kubwa ya kutokuaminiani miongoni mwa viongozi mmoja mmoja na kati ya kiongozi mmoja dhidi ya jumuiya

Mwaka 2022 kikosi cha kulinda amani cha EAC kilipopelekwa DRC, wajibu wao mkubwa ulikuwa kusaidia kuwaondoa M23 katika maeneo ya Kivu Kaskazini.

Hata hivyo, Kinshasa ilitaka kikosi hiki cha EAC kupigane na kudhoofisha kabisa M23. Kikosi cha EAC kiliposhindwa kufanya hivyo, muda wake wa awali ulipoisha, DRC haikuongeza mkataba, na badala yake ikakikaribisha kikosi cha SADC

Lakini Kigali imekuwa ikikikosoa kikosi cha SADC kilichopo nchini DRC. Inasema uwepo wake hapo si tu kwamba haulengi kuleta amani, bali ni wa maslahi ya kiuchumi hasa kuinufaisha Afrika Kusini

"SAMIDRC si kikosi cha kulinda amani, na hakina nafasi yoyote katika mgogoro huu. Kiliidhinishwa na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) kama kikosi cha kijeshi, kufanya oparesheni za kijeshi ili kuisaidia DRC kupigana dhidi ya watu wake wenyewe," amenukuliwa akisema Rais Paul Kagame

Kwa upande mwingine, Afrika ya kusini na Burundi imeilaumu Rwanda waziwazi kuchochea mgogoro huo kwa kuwasaidia waasi wa M23 na hata kuwa na wanajeshi wake nchini DRC, ili iendelee kunufaika kiuchumi. Shutuma hizi Rwanda inazikataa.

Lakini kuna changamoto ya rasilimali fedha ambayo inazikabili hizi jumuiya na kudhibiti uwezo wao wa kutekeleza majukumu yao kwa kiwango kinachotakiwa na kwa muda unaohitajika.

Katika mazingira ambayo kikundi cha M23 kinaendelea kuimarisha nafasi yao kisiasa miongoni mwa wananchi, hasa wa maeneo hayo ya Mashariki mwa Congo, nafasi ya jumuiya hizi kupata suluhisho ambalo litaifurahisha nchi mwanachama wake anayehitaji msaada, yaani DRC, ni ndogo.

Matumaini ya wengi ni kwamba ikatokea hizi jumuiya zikafanikiwa hata kuzishawishi pande zote kusimamisha mapigano kwa muda fulani, kurudi mezani kwa ajili ya mazungumzo na kurudisha maeneo muhimu huku Kivu ya Kaskazini chini ya udhibiti wa serikali, basi hayo yatakuwa ni mafanikio makubwa sana.

# Nguvu ya Mwanamke kujikwamua inaanzia ndani familia yake



Na Mwandishi Wetu

**MIPAKA ya kijinsia bado ipo kwenye jamii zetu.Na mbaya zaidi wanawake wanazingatiwa kama watu wa makundi maalumu. Mwanamke kuzingatiwa kama mtu wa kundi maalumu ndilo jambo linaloendeleza uwepo wa mipaka ya kijinsia katika fursa mbalimbali za kijamii ikiwemo fursa ya uongozi.**

Ukianzia kwenye ngazi ya shule watoto wa kike mara nyingi wanapatiwa misaada ya kujisitiri na mambo mengine kuliko watoto wa kiume kwahiyo hizo Hali zinaendelea kuwafanya wanawake waonekane kwamba wao ni wa makundi maalumu hivyo wanahitaji zaidi uangalizi wa wanaume na taifa Kwa ujumla.

Usawa hautakiwi kuwa wa upendeleo Bali kila binadamu anayetakiwa kuwa sawa na binadamu mwenzake basi awe sawa kiasili. Asili ndo itumike kuweka usawa lakini ikiwa kila siku tutaimba kuhusu kulazimisha fursa Kwa wanawake basi tutakuwa tunaendelea kuwafanya wanawake waonekane wao ni watu dhaifu kiasili.

Ili kuondoa changamoto zote zinazominya ushiriki wa wanawake kwenye masuala mbalimbali ya kijamii tuhakikishe tunaondoa misingi yote inayowaweka wanawake kwenye makundi maalumu na nafasi za upendeleo.Hakuna haja ya kulazimisha mada Bali kila jambo liwe kiasili na mabadiliko yaanzie kwenye familia zetu.

Hakuna namna mwanamke anaweza kuwa na nguvu kama mabadiliko hayataanzia kwenye familia yake.Wanawake kama wanataka kuwa kama wanaume na wawe sawa kwenye mambo yote ya kijamii na kitaifa basi waache unyonge na wasiwe wanapenda penda misaada na kuonekana kama wao ni kama watu wa makundi maalumu. Je wataweza?? Kazi kwao.

Uwezo kiakili na utendaji wa shughuli mbalimbali, wanawake wamekuwa wakionesha ufanisi mdogo sana na wengi wao wamekuwa wakiamini na kuwategemea wanaume katika kufanikisha shughuli hizo.Wanawake wenyewe wanawaamini sana wanaume kuliko wanavyojiamini wao wenyewe kwenye mambo mbalimbali yanayotegemea nguvu na akili.





# UJENZI BWAWA LA KIDUNDA KUMALIZA SHIDA YA MAJI












**MKURUGENZI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam(DAWASA)Mkama Bwire,pichani akizungumza na Waandishi wa Habari kuelezea mikakati ya Mamlaka hiyo kumaliza shida ya Maji Jijini Dar es Salaam na mikoa ya Pwani. Moja ya mikakati hiyo ni ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaondelea Mkoani,Ngerengere Morogoro.Picha nyingine tofauti ni Waandishi wa Habari,maofisa wa Dawasa,Mamlaka ya Bonde la Wami Ruvu,walipotembelea kujionea ujenzi wa mradi huo lakini pia kuo-**

# 4R ZA SAMIA DARASA KWA DEMOKRASIA TANZANIA



NA MWANDISHI WETU

ILIKUWA Januari 3 mwaka 2023.Dunia ilishuhudia kufunguliwa kwa siasa za vyama vingi na shughuli zake katika ardhi ya Tanzania, si kwa kauli bali vitendo hasa baada ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kuamua kuziishi kwa vitendo falsafa zake za 4R.

Jina la Rais Dk. Samia litaendelea kutajwa kwenye midomo ya wapenda haki, wanaojua maana ya uhuru wa kujieleza na kutumia mbinu za maridhiano kuleta maendeleo ya nchi.

Wakati wa vuguvugu la kuanza upya mfumo wa vyama vingi nchini mnamo mwaka 1992, mambo kama haya yalikuwepo, mivutano, maandamano, askari kuwazuia wafuasi wa vyama vya siasa kwa mabomu ya machozi, risasi bandia au virungu.

Katika uchaguzi wa kwanza wa vyama vya siasa mwaka 1995, kiongozi wa upinzani Augustino Lyatonga Mrema aliyegombea urais kwa tiketi ya Chama cha NCCR-Mageuzi ndio alikuwa na wafuasi wengi. Kauli zake zilisikika na kufuatwa na kundi kubwa la wananchi kwa wakati huo.

Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), walijawa hofu; wakaona dhahiri mgombea wao Benjamin William Mkapa hatafua dafu. Wakaenda kwa Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere kushitaki.

Majibu ya Mwalimu Nyerere yaliwanyong onyeza wote waliomfuata, ambao walilalamika Mrema anabebwa mabegani, akifika kwenye mkoa anatandikiwa khanga na gari kuzimwa huku akisukumwa.

Waliona hiyo ni ishara ya kuwavutia hata ambao walikuwa hawajui siasa ni nini wala nguvu au uwezo wa Mrema ni upi. Walitaraji majibu yatakayowapa faraja. Lakini Mwalimu aliwaambia kuwa Mrema aachwe abebwe, akasisitiza kuwa na yeyote anayetaka kubebwa kama maiti basi asizuiwe.

Masuala ya upinzani katika eneo lolote la nchi hayazuiliki, wakati Mwalimu Nyerere na wenzake wanapambana kupata uhuru wa Tanganyika kutoka kwenye makucha ya Waingereza katika miaka ya 1950; bado kulikuwepo na Waafrika waliozaliwa na kukulia Tanganyika waliunda vyama vya upinzani.

Baadhi ya vyama hivyo ni pamoja na African National Congress (ANC) cha Zuberi Mtemvu, All Muslim National Union of Tanganyika (AMNUT) ambacho kilikuwa chama cha Waislamu wazalendo wa Tanganyika pamoja na Tanganyika Democratic Party (TDP) cha Balozi Kasanga Tumbo huku vyama hivyo vikipewa nguvu na chama cha United Tanganyika Party (UTP) kilichoanzishwa na Gavana wa Tanganyika wakati huo Edward Twinning mwaka 1956 huku baadhi ya Waafrika wakiwa wanachama.

Utaona ni namna gani kina Mwalimu Nyerere walipata tabu kupambana na nguvu iliyotokana ndani yao (Waafrika),lakini baada ya kupata uhuru Disemba 9, 1961 na kufanyika uchaguzi wa vyama vingi baadaye, ilipofika mwaka 1965 Mwalimu Nyerere akiwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliamua kufuta mfumo wa vyama vingi nchini ili kuleta utulivu wa kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Baadaye kutokana na takwa la kimataifa Tanzania iliamua kurejea kwenye mfumo wa vyama vingi mnamo mwaka 1992.Hakuna kipindi kigumu katika uongozi wa Tanzania kama kuanzia mwaka 1992 hadi 2005. Mtikisiko mkubwa wa kisiasa ulipatikana, viongozi wa juu wakiongozwa na Mzee Ali Hassan Mwinyi (Rais wa Awamu ya Pili), Benjamin Mkapa (Rais wa Awamu ya Tatu) na baadaye Jakaya Kikwete (Rais wa Awamu ya Nne) walitumia uvumilivu wa hali ya juu kuhakikisha nchi inavuka salama; na walifanikiwa.

Hata hivyo, Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Pombe Magufuli alikuja na falsafa yake alitaka utulivu wa kisiasa ili afanye maendeleo. Alichoshwa na kelele za wapinzani kudai mambo ambayo pengine aliona hayana msingi. Akazuia shughuli za kisiasa kuanzia maandamano, mikutano ya hadhara isipokuwa kwa wabunge wa jimbo husika pekee.

Kwa kipindi chote cha uongozi wake madarakani kuanzia Novemba, 2015 hadi mauti yalipomkuta Machi 18, 2021. Tanzania haikuwa na vuguvugu la kisiasa. Ingawa minong ono ilikuwa mingi.

Dk. Samia Suluhu Hassan alichukua kijiti na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo Machi 19, 2021. Matumaini mapya yakaanza kuonekana kwenye sura za Watanzania hasa viongozi wa vyama vya kisiasa.Kila aliposimama kuzungumza na wananchi matarajio ni lini vyama vya siasa vitatoka kifungoni. Ndipo Januari 3, 2023 akatangaza kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini na kuondoa marufuku iliyokuwepo kwa muda mrefu.

Rais Dk. Samia kauli hiyo aliitoa mbele ya viongozi wa kitaifa wa vyama vya siasa alipowaita Ikulu ya Dar es Salaam, alisema: Uwepo wangu mbele yenu leo ni kuja kutangaza kwamba lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara sasa linaondoka. Hiyo ilikuwa habari njema mbele ya viongozi wa vyama vikuu vya siasa za upinzani nchini akiwemo aliyekua Mwenyekiti wa Chadema,Freeman Mbowe,Profesa Lipumba wa C.U.F na Zitto Kabwe wa ACT-Wazalendo.

Pengine tamko lile lilionekana na kawaida, lilionekana la kisiasa au kuondoa ungo juano, kama wasemavyo Waswahili. Lakini tukio la kuruhusiwa wafuasi wa CHADEMA kufanya maandamano kwenye jiji kubwa lenye shughuli nyingi kama Dar es Salaam, ilithibitisha haikuwa porojo.

Mjumbe wa zamani wa Kamati Kuu ya CHADEMA na mbunge wa zamani wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi alimpongeza Rais Dk. Samia wa uongozi wake wa maridhiano kwa kuruhusu maandamano.

Naye Mbowe, akaipongeza Polisi chini ya Rais Samia kwa ushirikiano wao kwa chama chake. Nalipongeza Jeshi la Polisi kwa busara hii. Karibuni Watanzania wote, tuandamane kwa amani, Mbowe amesema.Falsafa ya R4 (Reconciliation, Resilience, Reforms na Rebuilding of the Nation) ya Rais Samia imebadili upepo wa siasa nchini.

Haikuwa mara ya kwanza kwa Serikali ya Rais Samia kuruhusu maandamano ya upinzani. Mei, 2023, Polisi jijini Dar es Salaam waliruhusu maandamano ya Umoja wa Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) kwenda Ofisi za Bunge na kuwapatia ulinzi.

Kama hiyo haitoshi Rais Dk. Samia pia ameongeza uhuru wa wananchi wa kuongea, uhuru wa vyombo vya habari na asasi za kiraia.Wananchi kadhaa



# Wamarekani Waarabu watamuangusha Rais wa Marekani Donald Trump?



WAMAREKANI Waarabu na Waislamu walishiriki katika kumrejesha Donald Trump Ikulu ya White House.Ingawa asilimia yao nchini Marekani si kubwa, ushawishi wao ulikuwa mkubwa kwa sababu kuu mbili.

Kwanza ni mkusanyiko wao katika baadhi ya majimbo muhimu ambapo ushindani wa uchaguzi wa urais ulikuwa mkubwa, kama vile Michigan, na ya pili ni ukubwa wa ushawishi wa vyombo vya habari unaofurahia masuala yanayohusiana na Waarabu na Waislamu, hasa suala la Palestina na udhihirisho wake wa hivi karibuni katika vita vya Gaza.

Suala la kwanza bila shaka lilikuwa muhimu kwa Trump katika uchaguzi, huku la pili likiendelea kuwa muhimu huku urais wake unapoanza.Wamarekani Waarabu na Waislamu walishangazwa kusikia mawazo ya Rais Trump mapema katika kipindi chake cha urais, ambayo yalijumuisha uhamisho wa Wapalestina kutoka Ukanda wa Gaza huku Marekani ikiashiria kutaka kulichukua eneo hilo.

Huko Dearborn, Michigan, ambako wakazi wengi ni Waarabu, jiji hilo limekuwa kielelezo wazi cha ukuu wa Trump na kuwafikia wapiga kura Wamarekani, kushinda kura zao kwa gharama ya mpinzani wake wa chama cha Democratic Kamala Harris, Makamu wa Rais wa zamani Joe Biden. Biden alikuwa ameshinda zaidi ya theluthi mbili ya kura za wapiga kura wa Dearborn alipomshinda Trump mnamo 2020, lakini mambo yamebadilika sana miaka minne baadaye.

Niliposafiri na timu ya BBC hadi Dearborn na miji mingine ya Michigan nikiwa na habari za kampeni ya uchaguzi wa 2024, wakaazi wa Kiarabu walikasirishwa na utawala wa Biden-Harris, wakiulaumu na kuwajibika kwa vita vya Gaza na kuendelea kwake.

Miongoni mwao alikuwa Samra Luqman, mwanaharakati ambaye alikuwa Democrat na chama cha Biden lakini aliamua kumpigia kura Trump wa Republican kwa sababu alimlaumu Biden kwa kuhusika na vita vya Gaza na kushindwa kwake kuizuia Israel, alisema.

Aliniambia siku hiyo jinsi alivyoathiriwa na kuumizwa na vita vya Gaza, na pia aliniambia kuhusu mkutano wa moja kwa moja na Trump kupitia kampeni yake ya uchaguzi, ambayo aliwasiliana naye, licha ya kuwa alikuwa wa chama pinzani.

Trump, anasema, alichukua hatua ya kuzungumza naye na kumwambia juu ya hitaji la kusitisha vita, na hiyo ilichukua jukumu kubwa katika uamuzi wake wa kumpigia kura.

Ingawa Trump hakuwahi kuficha kuiunga mkono Israel, hata alipokuwa rais katika muhula wake wa kwanza wala wakati wa kampeni za uchaguzi, harakati zake kuwarai Waamerika Waarabu kumuunga mkono zilifanikiwa, kwani alizingatia wazo la ahadi yake ya kumaliza vita Mashariki ya Kati, na kwa madai kwamba vita hivyo havingezuka iwapo angekuwa rais.

Katika mazoezi, Trump aliitembelea Michigan mara kwa mara, na hata akaenda Dearborn yenyewe, ambapo wapiga kura wa Kiarabu walimsherehekea na kujibu ahadi zake za kumaliza vita na kuanza enzi mpya.

Mwishowe, Harris alipata pigo la kisiasa alipopata asilimia 37 pekee ya kura za wapiga kura wa Dearborn, huku Trump akipata asilimia 43 ya kura zao, na kura zilizosalia zikaenda kwa wagombea wengine.

Bishara Bahbah anasema anataka kumkumbusha Trump kwamba kuna uchaguzi ujao wa bunge, ambapo Chama cha Republican cha Trump kina wabunge wengi katika mabunge yote mawili, Baraza la Wawakilishi na Seneti.

Uchaguzi huo utafanyika mwishoni mwa mwaka ujao, na Bahbah anaeleza: "Trump atahitaji kura zetu ili chama chake kiendelee kudhibiti mabunge yote mawili ya Congress. Tupo hapa na bado hatujamaliza.

# Sam Nujoma: Mwanamapinduzi aliyeikomboa Namibia

**Aliheshimika na kufahamika kama "Baba wa taifa" na ishara ya mapambano ya kuikomboa Namibia. Maisha ya Sam Nujoma yalikidhi matarajio ya mtu mwenye hadhi kama yake kwa njia tofauti.**

Alipendwa na wengi kutokana na muonekano wake wa kuwa mchangamfu na mwenye tabasamu.

Alikuwa mtu wa watu iwe ni wakati ambapo alivaa nguo za kukimbia na kujiunga na raia wakifanya mazoezi katika barabara ya Independence Avenue katika mji mkuu wa taifa hilo Windhoek au wakati mwingine alipoamua kutotumia misafara rasmi ya magari.

Sasa, miongo minne baada ya kuiongoza Namibia katika vita vikali vya msituni dhidi ya serikali ya ubaguzi wa rangi ya Afrika Kusini hadi taifa hilo kupata uhuru, Nujoma amefariki akiwa na umri wa miaka 95.

Alifariki siku ya Jumamosi baada ya kulazwa hospitalini kwa muda wa wiki tatu alipokuwa akiugua, kwa mujibu wa tangazo la Rais Nangolo Mbumba, ambaye amesema kuwa kifo hicho "kimelitikisa" taifa.

Kupigania Uhuru

Shujaa huyu ambaye aliipa Namibia utambulisho wa kitaifa anaacha pengo ambalo ni wachache wanaoweza kulijaza.Namibia, awali ikifahamika kama South West Africa, ilipitia mateso kwa miongo kadhaa ikiwemo uporaji na unyanyasaji wa kikoloni chini ya mikono ya wazungu kutoka bara Ulaya ambao walifika nchini humo kwa wingi mwanzoni mwa karne ya 20.

Kuanzia mwaka wa 1904, wakoloni wa Ujerumani waliua maelfu ya raia wa Namibia katika kile kinachofahamika kama "mauaji ya halaiki yaliyosahaulika" duniani.

Maafisa wa Ujerumani walitumia Waafrika weusi kama mfano wa kufanyia majaribio katika uhalifu wa kutisha ambao baadaye ulitekelezwa na Wanazi wakati wa mauaji ya Wayahudi maarufu kama 'Holocaust' katika vita vya pili vya dunia.

Namibia ilikuwa chini ya ukoloni wa Wajerumani kutoka 1884 hadi 1915, wakati Ujerumani ilipopoteza koloni hilo katika vita vya kwanza vya dunia.Baada ya hapo Namibia ilikuwa chini ya utawala wa wazungu wa Afrika Kusini, ambao walitekeleza sheria zao za ubaguzi wa rangi nchini humo, na kuwanyima raia weusi wa Namibia haki zozote za kisiasa, pamoja na kuwanyima haki za kushiriki masuala ya kijamii na kiuchumi.

Kuanzishwa kwa sheria nyingi za ubaguzi wa rangi kulisababisha vita vya msituni kuzuka mwaka wa 1966, raia wa Namibia wakitafuta uhuru wa nchi yao.Kufikia wakati huu, Nujoma alikuwa tayari anahusika katika vita dhidi ya utawala wa wazungu waliokuwa wachache nchini humo.

Alipenda kujiita "mtoto wa kwanza katika familia maskini ya wakulima" kutoka kijiji cha kaskazini cha Etunda ambapo alianza maisha ya kawaida, akiwa na elimu ndogo tu ya shule ya msingi.

Alimuoa Kovambo Theopoldine Katjimune na pamoja wakajaliwa kupata watoto wanne, akafanya kazi kwenye shirika la reli, akiwa na shauku kubwa ya kujiunga na siasa na alitamani kuona watu wake wakiwa huru kutokana na dhuluma na aibu ya ukoloni.

Msukumo wake ulitokana na hadithi za viongozi wa awali wa upinzani wa Namibia, kama vile Hendrik Witbooi, ambaye alipigana dhidi ya Wajerumani katika miaka ya 1880.

Kufikia 1959, Nujoma alikuwa mkuu wa shirika la Owamboland Peoples organisation, vuguvugu la kupigania uhuru ambalo lilikuwa mtangulizi wa chama cha Swapo.

Mwaka mmoja baadaye, akiwa na umri wa miaka 30, Nujoma alilazimishwa kukimbia nyumbani na kwenda uhamishoni. Akiwa hana hati ya kusafiria, alitumia ujanja wake na kuchukua hulka ya watu tofauti ili kuingia kwenye treni na ndege – akafanikiwa kuingia Zambia na Tanzania kabla ya kuelekea Afrika Magharibi.

Kwa usaidizi wa mamlaka za Liberia ambao tangu zamani waliunga mkono azma ya Wanamibia weusi kutaka uhuru wao, Nujoma alisafiri kwa ndege hadi New York na kuomba Umoja wa Mataifa kusaidia kuipa Namibia uhuru wake - lakini Afrika Kusini ilikataa kufanya hivyo.

Nujoma alitajwa kuwa "gaidi wa ki-Marxist" na viongozi wa wazungu wa Afrika Kusini kwa kuongoza vikosi vilivyopigana pamoja na vuguvugu la kupinga ubaguzi wa rangi, na kusababisha changamoto kubwa kwa utawala dhalimu katika nchi kadhaa za kusini mwa Afrika.

Akisaidiwa na wanajeshi wa Cuba waliokuwa wakipigana katika nchi jirani ya Angola, wapiganaji wa msituni wa Swapo walishambulia kambi za Afrika Kusini nchini Namibia.

Aliporejea kutoka uhamishoni, Nujoma alikamatwa tena na mamlaka za Afrika Kusini na kusafirishwa hadi Zambia miaka sita baadaye.

"Tulijua kwamba ni nguvu za kijeshi tu na uhamasishaji mkubwa wa kisiasa wa watu ambao ungeilazimisha Afrika Kusini kuondoka Namibia," Nujoma alisimulia katika wasifu wake wa Where Others Wavered, uliochapishwa mwaka 2001.

Aliongoza vikosi vya Swapo kutoka uhamishoni, kabla ya kurejea nchini mwaka 1989, mwaka mmoja baada ya Afrika Kusini kukubali kuikabidhi Namibia uhuru wake.

Afrika Kusini ilikuwa ikitengwa zaidi kimataifa na gharama ya kijeshi ya kushiriki vita ilikuwa ikiongezeka. Hatimaye Namibia ilipata uhuru mwaka 1990 baada ya takriban miaka 25 ya vita.

Kujenga taifa

Katika uchaguzi wa kwanza wa kidemokrasia nchini Namibia mwaka 1990, Swapo ilipata kura nyingi zaidi na Nujoma akawa rais wa kwanza wa nchi hiyo. Nujoma alijali sana maslahi ya watoto, na alianzisha malipo ya kuwatunza yaliyowalazimu akina baba waliowatelekeza watoto wao kuchangia gharama za malezi.

Pia alitetea maendeleo ya wanawake, na kusaidia kubadilisha itikadi za mfumo dume ambazo ziliwafukuza wajane kutoka kwenye ardhi za familia mara tu waume zao walipofariki.Pia alihakikisha juhudi za maendeleo zinaungwa mkono na wafadhili wa kimataifa.

Nujoma alichaguliwa tena kwa mihula miwili zaidi mwaka 1994 na 1999 – alipokosolewa kwa kubadilisha katiba ili aweze kugombea muhula wa tatu madarakani.Alipokosolewa kwa mtindo wake wa uongozi au kuhojiwa kuhusu vitendo vya hapo nyuma vya chama chake cha kisiasa, tabasamu lake pana liliweza kugeuka na kuwa mkali.

Wakati mwingine angemnyooshea kidole yeyote aliyethubutu kuhoji au kukosoa waziwazi masuala hayo na kuna wakati fulani ambao angerusha matusi. Alichukia waziwazi mahusiano ya watu wa jinsia moja, lakini hakuwahi kufikia hatua ya kubadilisha katiba au sheria ili kuyafanya kuwa haramu.

Nujoma daima alithamini urafiki wake wa karibu na Robert Mugabe wa Zimbabwe, lakini kama rais wa Namibia aliepuka uchokozi wa hadharani dhidi ya wakosoaji wake.Hata hivyo angetumia mifumo ya Swapo kutoa shinikizo kwa mwananchi wa kawaida kutii chama chake na pia kuruhusu chama hicho kutumia fedha za serikali ili kuhakikisha utawala wake unaendelea.

Alikuwa na uwezo mkubwa,ikiwemo kuamuru baraza lake la mawaziri la Nujoma kufikia maamuzi badala ya wote kushiriki mijadala ili kuamua jambo. Alipoondoka uongozini mwaka 2005 na baadaye kama rais wa Swapo mwaka 2007, baada ya kuhudumu kama kiongozi wa chama hicho kwa miaka 47 - alikabidhi madaraka kwa mrithi wake, Hifikepunye Pohamba.

Hata baada ya kuondoka madarakani, Nujoma bado alikuwa na ushawishi mkubwa kwa maamuzi ya chama na serikali. Hata hivyo mafanikio yake akiwa madarakani yako wazi, wananchi wengi wa Namibia wakimsifu kwa kuongoza nchi hiyo kujikita kwenye utawala wa kidemokrasia.

Tangu uhuru wake, Namibia imeonekana kuwa mojawapo ya mataifa yenye hadithi za mafanikio barani Afrika, kwasababu ya kuandaa chaguzi za mara kwa mara za amani na demokrasia.Na licha ya udhalilishaji na dhuluma za wakoloni weupe dhidi ya raia weusi wa Namibia, Nujoma alishikilia katiba ya nchi hiyo katika kulinda haki za kimsingi za Wanamibia wote bila kubagua kabila wala rangi yao.

Sera ya umoja wa kitaifa iliwashawishi wazungu nchini humo kusalia na bado wanaendelea kutoa mchango mkubwa katika kilimo na sekta nyingine za kiuchumi.Uwezo wa Nujoma wa kuunganisha taifa la watu milioni tatu - kutoka jamii 10 tofauti ulimfanya kupendwa na wengi.

Kwa kutambua mafanikio yake makubwa, bunge la Namibia lilimpa hadhi rasmi ya "Baba Mwanzilishi wa taifa la Namibia" mwaka 2005.Pia alipata tuzo nyingi za kimataifa kama vile Tuzo ya Amani ya Lenin,Tuzo ya Amani ya Indira Gandhi na Tuzo ya Amani ya Ho Chi Minh.

Katika miaka yake ya mwisho,Nujoma hakuonekana sana hadharani, akipendelea kutumia wakati mwingi akijumuika na familia yake kubwa.Anakumbukwa kwa haiba yake na maono yasiyoyumba – akiwa baba sio tu kwa familia yake bali kwa taifa zima.



# WACHENI KIBABAGE AOGELEE KWENYE BAHARI YAKE






Na Hilary Rocks

MDOGO na rafiki yangu Nickson Kibabage ndiye beki bora wa kushoto tuliyenaye Tanzania kwa sasa.Amekomaa. Ni vile katokea kwetu Morogoro nauli haizidi 15,000.Na hajapanda ndege kuja jijini Dar es Salaam kwa wajuaji.

Napenda wachezaji wa kigeni waje kwenye ligi yetu kuja kuwachangamsha wachezaji wetu ili wasibweteke. Lakini napenda mchezaji wa kigeni anayesajiliwa kuja kugombania namba na mchezaji mzawa basi awe na uwezo mara mbili ya mzawa.Kwa sasa ndani ya Yanga kuna vita kali ya namba kati ya Kibabage na Shadrack Bocca.

Kibabage alianza kumtikisa Joyce Lomalisa raia wa Congo aliyetimka msimu uliopita na sasa anakula sahani moja na Shadrack Bocca.Haitaji hata akili nyingi kujua hili kama kinda huyo ndiye mmoja ya mabeki bora katika soka letu.

Ukweli ni kwamba kijana kwa sasa ana uwezo mkubwa sana.Ukiangalia nguvu na kasi aliyonayo katika kusaidia mashambulizi yaani ni Modern Fullback.

Akiongeza ... ub-
o ... ra
kwenye kuwa ... na
nidhamu ... ya
eneo la ki- ... ulin-
zi hana mp- ... in-
zani nchini.

Kila siku kiwango chake kimekua kikimarika zaidi. Kibabage wa Singida Big Stars na huyu aliye Yanga ni watu wawili tofauti.Hawafanani. Wameachana vitu vingi ndani ya uwanja.Huyu aliye Yanga ni bora sana. Amekomaa na kiwango chake kimeimarika kwa kiasi kikubwa.Hata ikitokea wamekutana barabarani watapishana kwani kila mmoja ni ngumu kumtambua mwenzake.

Ndani ya kikosi cha Yanga amejitengenezea nafasi yake machoni mwa kocha Miguel Gamondi kumuamini kumpa nafasi ya kuanza kucheza.Kama kuna eneo ndani ya kikosi cha Yanga ambalo mashabiki wa timu hiyo hawana wasiwasi nalo ikitokea ShadrackBocca hayupo basi ni kwenye mbavu ya kushoto.

Mbadala wa Bocca ni Kibabage.Kijana amejiweka kwenye ubora wa kupokezana namba raia huyo wa Congo DRC.Ni suala la muda tu.Ndani ya uwanja wa mazoezi Kibabage anafanya mambo mengi ya kumuweka fiti ili asiwe msugua benchi.

Benchi la Ufundi la Yanga ni kama limegundua wawili hao ni kama wanasifa za kuanza kikosi cha kwanza na makocha wote aliokutana nao Kibabage ndani Yanga wamekuwa wakiwatumia kwa mpangilio unaonesha kuwa ni walinzi sahihi wa Yanga.

Zitazamee baadhi ya mechi za Yanga utagundua kuna kitu Kibabage amekitengeneza kati yake na Mudathir Yahaya. Wametengeneza kitu cha hatari sana.Mudathir anajua mikimbio sahihi ya Kibabage na anajua akae sehemu gani ili pasi atakayotoa mwanae impate kirahisi sana.

Kibabage ni hatari sana kwenye kushambulia,kasi yake leo iliwahi kumshinda Clement Mzize kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC.Alhamdulilah Yanga walishinda mabao 3-0.Mzize alipishana sana na Kibabage wakati anajenga mashambulizi. Kwa kasi yake Mzize alibaki nyuma na kuzikosa pasi za kijana wa Morogoro Kibabage.

Uwanja wa mazoezi pale Avic Town bila shaka ndo jiko pekee linalotengeneza bond hii ya Mudathir na Kibabage.Kuna mechi moja pale Chamazi walitokea benchi wote wawili, Kibabage alitengeneza nafasi na Mudathir akaweka kambani na akafanya hivyo dhidi ya KMC mwenzie akawekaka nyavuni.The Rocky star (A skilled writer).

FIKRAPEVU
MICHEZO
JUMATATU FEBRUARI 10, 2025



# Vita ya ubingwa Simba,Yanga bado mbichi

Na Husna Nassoro

VITA ya kuwania alama tatu muhimu kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara inaendelea tena leo kwa Mabingwa watetezi Yanga,kukaribishwa na Maafande wa JKT Tanzania wakati kesho Simba watakuwa wenyeji wa Tanzania Prisons uwanja wa KMC Kinondoni.

Yanga watashuka uwanja wa Meja Isamuyo kuwavaa JKT wakipania kuvuna pointi tatu ili kuzidi kujikita kileleni kwa msimamo.Ikumbukwe Yanga wanaongoza Ligi hiyo wakiwa na pointi 45 kibindoni wakifuatiwa na Simba yenye alama 44 na kufanya vita ya kuwania ubingwa msimu huu kunoga mapema.

Yanga itaingia katika mchezo huo ikiwa inataka kuendeleza moto wa ushindi ilionao ambapo mechi iliyopita iliichakaza Fountain Gate mabao 6-1.Kwa upande wa Simba wataingia katika mchezo huo wakiwa na hasira ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Singida Fountain Gate mchezo uliopita na hivyo hawatataka kufanya makosa tena mbele ya Tanzania Prisons.

Mpaka sasa Simba na Yanga zimeshajikatia kipande chao cha mbio za ubingwa huku wakiiacha Azam FC ikijikongoja taratibu na pointi zake 39 kusubiria vigogo hao mmoja ateleze.

## Yanga yamrejesha Kocha wa viungo

Na Yassir Sudi

UONGOZI wa klabu ya Yanga umemrejesha kwenye benchi la Ufundi aliyekuwa Kocha wa viungo wa timu hiyo Taibi Lagrouni (52) raia wa Morocco.


Tabi amerejea kwenye kikosi cha Yanga kuendelea kutumikia mkataba wake kama kocha wa viungo ambapo aliwekwa kando baada ya ujio wa aliyekua Kocha wa timu hiyo Sead Ramovic aliyekuja na kocha wake wa viungo Adnan Behlulovi.

Ofisa wa habari wa Yanga,alithibitisha ujio wa Kocha huyo akisema ni sehemu ya maboresho ya benchi la Ufundi kufanya mambo makubwa katika Ligi Kuu na michuano mingine ambayo timu hiyo inashiriki.






## Harry Kane atajwa Arsenal



Mshambulizi wa Uingereza Harry Kane,31,amekataa kuzungumza kuhusu ripoti kwamba anaweza kuhamia Arsenal mwaka ujao,kwa sababu ya kipengele cha kutolewa katika kandarasi yake ya Bayern Munich. (Mirror)